

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA

SHULE YA SEKONDARI MWAKILANGI

MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE

Mkuu wa shule mwakilangi sekondari anafuraha kukujulisha kuwa wewe _____ umechaguliwa kujiunga na shule hiyo kidato cha kwanza mwaka _____. Hivyo natumia nafasi hii kukukaribisha sana.

Shule ya sekondari Mwakilangi iko katika kata ya kinang'weli, kijiji cha mwakilangi kilometa 3 toka senta za Mahembe na Sawida. Shule iko katika wilaya ya Itilima, Mkoa wa Simiyu.

Shule itafunguliwa tarehe _____, hivyo unatakiwa ujia mapema na ufike shuleni siku hiyo na kuripoti katikati ofisi ya Mkuu wa shule au Makamu mkuu wa shule ili usajiriwe kwenye kitabu cha shule.

Lugha inayotumika shuleni kwa mawasiliano ni kiingereza (English language) hivyo hakuna lugha nyingine itakayo tumika kwani lugha hiyo ndiyo imebeba masomo yote isipo kuwa somo la Kiswahili, hivyo ni rahisi sana jia vizuri, na walimu tutakusaidia.

MAHITAJI YA SHULE:

1. SARE ZA SHULE: (i) Sketi Mbili Nyeusi 1 na Bluu bahari 1, (kila sketi iwe na tai yake) kwa wasichana. Sketi lazima iwe ndefu kitambaa kizito, Iguse jicho la mguu, na iwe na Marinda.
(2) Suruali mbili Nyeusi 1, Bluu 1 kila suruali iwe na tai yake, Isiwe paipu wala modo, lazima iwe na rinda na ufito chini Miguuni walau 20-21.
(3) Shati kwa wote 2 nyeupe na wavulana singiledi nyeupe na wasina shumizi (vibode) nyeupe, kisiwe cha rangi nyingine.
(4) Viatu Vyeusi V yenye sori fupi na soksi Nyeupe kwa wasichana Mbili na nyeusi kwa wavulana pea mbili.

5. Sare za michezo- Wavulana kaptula na T-sheti nyeupe na viatu vya michezo raba ni

Lazima – Wasichana trakisuti za bluu na viatu raba ni lazima

6. DAFTARI: Shule inafundisha masomo tisa, lakini kutokuwa na mafunzo kiingereza ya wiki

Sizizo pungua nne, hivyo ni vyema uje na daftari za kutosha zisizopungua tisa,

Ukipata counter book ni vizuri zaidi.

NB: Ili kutunza unadhifu na hadhi ya kusoma sekondari kama utaweza ni vizuri kuwa na begi la

Kubebea vifaa vyako vya shule, siyo Bob male zenye picha ya uvutaji bangi wa sigara na

Kadhali, Pia uje na kamusi (dictionary) English to English.

Utakapo kuja shuleni hakikisha unapita kwenye zahanati au kituo cha Afya kujua hali ya afya yako ili utuletee taarifa hizo, zitasaidie karika kutunza na kukulea vema kulingana na hali utakayokuwa nayo.


Aidha shule inaamini **Nidhamu, juhudi na mahudhurio** yako shuleni ndizo nguzo za mafanikio ya masomo yako. Sheria kanuni na taratibu za shule kama zilivyowekwa na Wizara ya Elimu, sayansi na teknolojia, Halmashauri ya Wilaya ya Itilima Idara ya Elimu Sekondari, Mkoa wa Simiyu kitengo cha Elimu na shule, utazipata mara utakapofikia shuleni tarehe _____.

Tafadhali zingatia muda uliopangwa wa kuripoti shuleni, vinginevyo hatua za kisheria zitachukuliwa kwa Mzazi au Mlezi atakae kwamisha malengo hayo..

Karibu sana Mwakilangi Sekondari, Walimu wapo wakutosha na wanafundisha vizuri sana, hivyo ni Kisiwa cha Amani na Upendo na mwanafunzi ukifika shuleni tu, tayali umeshafaulu katika masomo Yako.

Nakutakia afya njema, Mungu akutangulie na tuonane January 2020.

Wako:



CYPRIAN E. NDISANYE

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MWAKILANGI
S. L. P. 52
BARIANI